



**OREGON
DEPARTMENT OF
AGRICULTURE**



Idara ya Kilimo ya Marekani (USDA), Huduma za Masoko ya Kilimo (AMS) zimeingia katika makubaliano ya ushirikiano pamoja na Idara ya Kilimo ya Oregon ili kusimamia mpango huu.

Ruzuku ya Miundombinu ya Mfumo wa Chakula Endelevu

Mpango wa Miundombinu ya Mifumo ya Chakula Endelevu (RFSI) unalenga kujenga uthabiti kati ya ugavi na kuimarisha mifumo ya chakula ya ndani na kikanda kwa kuunda njia mpya za mapato kwa wazalishaji wa Oregon.

Fedha zitasaidia kupanua uwezo na miundombinu kwa ajili ya kujumlisha, usindikaji, kutengeneza, kuhifadhi, kusafirisha, kuuza kwa jumla na usambazaji wa bidhaa za chakula zinazozalishwa nchini na kikanda, ikiwa ni pamoja na mazao maalum, maziwa, nafaka za kutumiwa na binadamu, ufugaji wa samaki, na bidhaa zingine za chakula, isipokua nyama, kuku na dagaa waliovuliwa porini.

ODA itapea kipaumbele miradi ya ufadhili inayonufaisha mashamba madogo yanayochipuka pamoja na biashara za chakula kutoka kwanye vikundi ambavyo vimekua na shida katika historia.

Washirika Wanaostahiki

- ✓ Wazalishaji wa kilimo au wasindikaji, au vikundi vya wazalishaji wa kilimo na wasindikaji
- ✓ Taasisi kama vile shule, au hospitali zinazoleta wazalishaji pamoja ili kuanzisha miundombinu ya ushirika au kuwekeza katika vifaa ambavyo vitafaidi shughuli nyingi za wazalishaji ambao wako katikati ya ugavi kama vile usindikaji, ujumlishaji, usambazaji wa bidhaa za kilimo zinazolengwa
- ✓ Vyombo vya serikali za mitaa vinavyofanya kazi kwenye ugavi kama vile usindikaji, ujumlishaji, na usambazaji wa bidhaa za kilimo zinazolengwa
- ✓ Mashirika yasiyo ya faida yanayoendesha shughuli za kati ya ugavi kama vile usindikaji, ujumlishaji na usambazaji wa bidhaa za kilimo zinazolengwa

Ruzuku ya Ufuatiliaji	Miundombinu	Vifaa vilivyorahisishwa Pekee
Vipaumbele	<p><i>Ittoa kazi bora inayosaidia familia pamoja na matibabu/usalama wa wafanyikazi</i></p> <p><i>Itazingatia biashara ndogo na za kati zinazoongeza uchaguzi na chaguo kwa watumiaji na wazalishaji (mkazo wa kuongeza thamani)</i></p> <p><i>Onyesha usaidizi wa ndani kwa mradi</i></p> <p><i>Saidia jamii ambazo hazijahudumiwa vyema</i></p> <p><i>Huwasilishwa na vyama vya ushirika, biashara zinazomilikiwa na wakulima na wafanyakazi</i></p> <p><i>Kusaidia mapendekezo ambayo hutoa bei nzuri, mishahara ya haki, na nafasi mpya za kazi salama ambazo huweka faida katika jamii za vijijini.</i></p> <p><i>Ongeza utofauti katika chaguzi za usindikaji kulingana na mbinu za muundo wa biashara, jiografia, na upatikanaji kwa jamii ambazo hazijahudumiwa</i></p> <p><i>Pangilia na malengo ya Kituo cha Biashara cha Chakula cha Mkoa cha Kaskazini-magharibi na Rocky Mountain</i></p>	
Mifano ya miradi inayokubalika (hii sio orodha kamili)	<p><i>Kuboresha utengenezaji, ufuatiliaji, uhifadhi na mifumo ya teknolojia ya habari</i></p> <p><i>Imarisha usalama wa wafanyikazi kwa kutumia teknolojia mpya au uwekezaji katika uboreshaji wa kituo</i></p> <p><i>Kuboresha uwezo wa taasisi kutii mahitaji ya shirikisho, jimbo na usalama wa chakula nchini</i></p> <p><i>Kuboresha shughuli kupitia fursa za mafunzo na Kusaidia katika ujenzi wa kituo kipyaa</i></p> <p><i>Kuboresha au kupanua kituo kilichopo (pamoja na upanuzi na marekebisho ya majengo yaliyopo na/au ujenzi wa majengo mapya katika vituo vililoipo.</i></p>	<p><i>Kuboresha vifaa vya usindikaji na utengenezaji wa kisasa</i></p> <p><i>Kuunda, kubinafsisha au kusakinisha vifaa vinavyopunguza utoaji wa gesi chafu, kuongeza ufanisi katika matumizi ya maji, kuboresha ubora wa hewa na/au maji, na/au kufikia lengo moja au zaidi la hatua za hali ya hewa za USDA.</i></p> <p><i>Imarisha usalama wa wafanyikazi kwa kutumia teknolojia mpya au uwekezaji katika uboreshaji wa vifaa</i></p> <p><i>Kuboresha uwezo wa taasisi kutii mahitaji ya shirikisho, jimbo na usalama wa chakula nchini</i></p>
Kipindi cha ombi	Januari 1 - Februari 29, 2024	Februari 1 - Februari 29, 2024
Kiasi cha tuzo	\$100,000-\$2,000,000	\$10,000 - \$100,000
Tarehe inayotarajiwa kuanza	Agosti 2024	Agosti 2024
Bidhaa Zinazostahiki	<i>Matunda, Mboga, Karanga za miti, Matunda yaliyokaushwa, Maziwa, Nafaka za kutumiwa na binadamu, Ufugaji wa samaki, na bidhaa nyingine za vyakula isipokua nyama, kuku na dagaa waliovuliwa porini.</i>	

Kwa habari zaidi tafadhali wasiliana:

Gabrielle Ugalde
 Mratibu wa Mpango wa Ruzuku ya Mazao
 Maalumu
 Upatikanaji wa Soko na Udhhibitisho
 Barua pepe:
 ResilientSystemGrant@oda.oregon.gov Simu:
 503-986-6473
 Simu Mbadala: 541-913-3440
 Ukurasa wavuti: oda.direct/rfsi

10/2023

